**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OWM-TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA MJI RUFIJI**
**SHULE YA SEKONDARI RUFIJI**

**Mkuu wa Shule +255718285764 /0625110833**

**Makamu Mkuu wa Shule +255678194846**

**Shule ya Sekondari Rufiji**

**S.L.P. 62 Ikwiriri – Rufiji**

**Tarehe ....................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI RUFIJI. HALMASHAURI YA MJI RUFIJI MKOA WA PWANI MWAKA …...**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya **............................................**

Shule ya Sekondari **RUFIJI** ipo umbali wa Kilometa **160** Mashariki mwa Mji wa **DAR ES SALAAM** Usafiri wa basi kutoka mjini **MBAGALA** unapatikana katika kituo cha mabasi **MBAGALA RANGI TATU** Nauli ni Shilingi **8,000**/= kituo kinaitwa **MZAMBARAUNI** utatembea kwa umbali wa km 01 mpaka shuleni Na kwa wanafunzi wanaotoka Mikoa ya kusini (Lindi na Mtwara) washuke kwenye stendi ya **IKWIRIRI**, Kisha watafute usafiri wa Kwenda **RUFIJI SEKONDARI** wataletwa kwa bodaboda kwa shilingi elfu tatu**.**

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **……….**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……….** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **………….**
Mwanao atapokelewa shuleni endapo atasoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata A-G vifuatavyo **;**

A. Maelekezo ya kujiunga na shule (joining instructions)
B. Vitabu viivyopendekezwa na TIE.
C. Michango mbalimbali ya shule.

D. Maelezo binafisi ya mwanafunzi.
E. Fomu ya kupimwa toka kwa mganga(Medical doctor).
F. Ahadi/kiapo cha mwanafunzi.
G. Sheria na kanuni za shule.

Ni matumaini yetu kwamba mwanafunzi atasoma na kuzingatia maelekezo yote na mzazi/mlezi utamtimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.

**A. MAELEKEZO MAALUM YA KUJIUNGA NA SHULE**

**Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni **Suruali mbili kijivu mpauko (Dark grey).** Maelezo ya mshono: **iwe na marinda mawili mbele na chini iwe na turn up/mkunjo wenye upana wa cm 1**.
ii. Mashati **rangi nyeupe yenye mikono mirefu mawili.**
iii. Sare ya Michezo ni **track suit 01 rangi ya blue ya shule (classic blue)**.
iv. Viatu vya shule jozi 02 vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wenye bakozi ndogo wa kuvalia suruali.
vii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) **Suruali mbili rangi nyeusi (black).**
viii. T-shirt mbili za kola zenye nembo ya shule rangi **ya damu ya mzee (maroon).** (Zinapatikana shuleni kwa anayehitaji).
ix. Tai rangi ya nyeusi.
x. Raba rangi nyeupe za michezo.

Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

**i.** Madaftari **Counter books quire 3 yasiopungua 10.**
**ii.** **Ream (A4)** tatu ( 3 ) kwa mwaka;
**iii.** **Picha nne (4**) passport size akiwa amevaa shati jeupe na rangi ya blue nyuma ya picha
**iv.** Scientific calculator kwa wote na graph pad moja kwa wanaosoma geography.
**v.** Godoro la futi 2.5 x 6.
**vi.** Mashuka rangi ya sky blue jozi 2, foronya ya godoro (bed cover) nyeupe 1, foronya za mto light blue, mto na chandarua rangi nyeupe kimoja.
**vii.** Nguo za ndani (boksa) nusu dozen.
**viii.** Kandambili(bata/bora) kwa ajili ya kuogea na sandal za kimasai zisizo na urembo kwa ajili ya kushindia.
**ix.** Vyombo vya chakula (sahani,bakuli,kikombe na kijiko au bakuli kubwa lenye mfuniko(container).
**x.** Ndoo kubwa mbili zenye mifuniko (lita 20).
**xi.** Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili (tranker).
**xii.** Kwanja 1,jembe 1,reki 1 na fagio 2 za ndani na wachelewa la wima(mmoja) lenye mpini (**Kama unatoka mikoa ya mbali njoo shuleni utaelekezwa vinapouzwa kuepuka usumbufu kwenye mabasi na daladala wakati wa kusafiri kuja shuleni**)
**xiii.** Urefu wa mwanafunzi (Ft)……… uzito wa mwanafunzi (kg)…………….

**B.Vitabu vya masomo ya tahasusi vilivyopendekezwa na TIE,**

1. **CHEMISTRY (kwa wanaosoma PCM pekee)**

- ➢ Modern chemistry ABC Of class XI Part I & II By Dr. S.P Jauhar
- ➢ Modern chemistry ABC Of class XII Part I & II By Dr. S.P Jauhar
- ➢ Essential of Physical Chemistry class XI & XII by Chand.
- ➢ Advanced Physical Chemistry by Ngaiza Lusima (2014)
- ➢ Conceptual Chemistry for Class XI by S.K. Jain.
- ➢ Comprehensive Chemistry volume I class XII by Dr. N.K. Verma , S.K. Khanna & Dr. B .Kapila.
- ➢ Advanced Organic Chemistry by Arun Bahil, S. Chand.

**2.PHYSICS ( kwa wanaosoma PCM pekee)**

- ➢ Physics for Advanced level secondary schools ,students book form five by TIE.
- ➢ Physics for Advanced level secondary schools, students book Form six by TIE.
- ➢ Principles of physics for class XI, V.K Mehta, S.Chand.
- ➢ Principles of physics for class XII, V.K Mehta, S.Chand.
- ➢ Modern ABC of physics for class XI part I & II by Satish K. Gupta.
- ➢ Modern ABC of physics for class XII part I & II by Satish K. Gupta.

**3. ADVANCED MATHEMATICS**

- ➢ Pure mathematics 1 ( 4th Edition 1985-j.k Backhouse)
- ➢ Pure mathematics 2 (3rd Edition 1985- j.k Backhouse)
- ➢ Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools Form V by Septine i. Sillem (2015)
- ➢ Advanced Mathematics for Advanced Secondary School Form VI by Setine I. Sillem.
- ➢ Conceptual Advanced Mathematics For Secondary Schools Form V by P.L.mayombya.
- ➢ Conceptual Advanced Mathematics For Secondary School Form VI by P.L.Mayombya**.**

**3.GEOGRAPHY (Kwa wanaosoma EGM).**

- ➢ Integrated Approach in Geography by David Waugh (2009) 3rd Edition
- ➢ A Comprehensive Approach in Physical Geography by D.T.Msabila (2018)
- ➢ Practical Geography by Zisti Kamili 2nd Edition 2016.
- ➢ Complementary Physical Geography for secondary schools by O. Mpalaki & F. Lighuda.

- ➢ Affordable Edition for Advanced leaners by Zisti Kamili.

**4.ECONOMICS (Kwa wanaosoma EGM).**

- ➢ Economics 1 & 2 by Tayebwa Mgisha.
- ➢ Modern Economics Theory by Dewelt.
- ➢ Essential Economics 1 & 2 by Odhiambo.
- ➢ Modern Economics 20th Edition by Ahuja.
- ➢ Comprehensive of Economics Questions and Answers by Tayebwa.

**C.MICHANGO MBALIMBALI.**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

- Michango yote ya shule ilipwe kwenye akaunti namba **21310054424 NMB BANK** jina la akaunti ni **RUFIJI SECONDARY SCHOOL CAPITATION ACCOUNT.**

**NB:** Kuwa makini katika kuweka fedha za michango kwenye akaunti husika na si vinginevyo. Hatutahusika na uzembe wowote wa kuchanganya malipo katika akaunti za shule. Jina la mwekaji liwe la mwanafunzi na si mzazi/mlezi. Mwanafunzi aje na **PAY SLIP** ya benki wakati wa kuripoti.na atoe kopi ya PAYSLIP na abaki nayo kama kielelezo chake.

**D.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**D. 1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

**Mwanafunzi hapaswi kuja na simu au laini ya simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)**.

- **Mwanafunzi anatakiwa kufungua akaunti yake binafsi ya benki CRDB au NMB kwa ajili ya kutunza fedha zake za nauli na matumizi yake madogo madogo, ukija shule utaelekezwa namna ya kufungua , uje na picha za passport size mbili na kitambulisho cha kupigia kura au namba ya nida kama unayo.Pia unatakiwa kuwa na bima ya afya CHF au NHIF.**

- **Jumapili ya Mwisho wa mwezi ndiyo siku ya wanafunzi kutembelewa na Ndugu(visiting day)**

- **Shule ya sekondari Rufiji inayomaabara ya kompyuta kwaajili ya kila Mwanafunzi kujua kutumia na kusomea,hivyo mwanao atakiwa ajifunze kutumia kompyuta akiwa shuleni.**

**D. 2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;

vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.


**E.Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.


**F.**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**JAMES D. MAYUNGA**



MKUU WA SHULE




**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama**

**walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO**
**USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0718 285764 (mwl. James D. Mayunga)**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0678 194846(mwl. Mariam K. Mambo)**
- **Mwalimu wa Taaluma 0676934 142 Mwl Shemsuu**
- **Mwandamizi Taaluma 0752306644 (mwl. Gervas M. Mmbaga)**
- **Mwandamizi Malezi 0766340909(mwl. Jackline S. Anthony)**

**Fomu Na.1**

## KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ……………………………………………………………………. Ambaye nimechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Rufiji kidato cha …………….. mwaka …………… ninaikubali na kuipokea nafasi hii niliyopewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na shule ya Rufiji sekondari.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Ninaamini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa nikiwa hapa shuleni

1. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu
2. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara.
3. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapa shuleni
4. Ikiwa nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/mlezi wangu ………………………………………………….. (jina la mzazi)kwa ajili ya hatua stahiki za kinidhamu

Sahihi ya mwanafunzi …………………… tarehe ……………………

**<u>Fomu Na.2</u>**

**KIAPO CHA MZAZI/MLEZI**

Mimi………………………………… wa S.L.P ……………Mji .......................Simu Na……………………..…ninakubali mtoto wangu …………………………………….

Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Rufiji mwaka ………… ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyokatika maagizo ya kujiunga na shule . ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu watatu (3) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni,

PICHA YA NDUGU WA KWANZA

**JINA ………………………………. KAZI………………………MAKAZI…………..… SIMU …………………………SAHIHI…………………...**

**Uhusiano na mwanafunzi ………………………………………………………..**

PICHA YA<br>NDUGU WA<br>PILI

**JINA ………………………………. KAZI………………………MAKAZI…………..… SIMU …………………………SAHIHI…………………...**

**Uhusiano na mwanafunzi ………………………………………………………..**

PICHA YA<br>NDUGU WA TATU

**JINA ………………………………. KAZI………………………MAKAZI…………..… SIMU …………………………SAHIHI…………………...**

**Uhusiano na mwanafunzi ………………………………………………………..**

**PRESIDENT OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRAN AND LOCAL GOVERNMENT (PO-RALG)**

**RUFIJI TOWN COUNCIL, RUFIJI SECONDARY SCHOOL**

P.O.BOX 62,

IKWIRIRI – RUFIJI,

DATE: **..............................**

**STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM**

**To the medical Officer**

**……………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………………**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF ……………………………………….**
**FORM …………. YEAR ………**
**Please examine the above named as to his fitness for admission to school as a student.**

***Name and signature of requesting officer***
**Name ……………………………………….. Signature ……………………**
**Date ………………………**

**(*To be completed by a medical officer*)**
**I have examined the above named and she/he has found with**
**……………………………………………………………………………………………………**
**…………………………………………………………………………**
**I consider that he/she-- is physically fit/unfit to pursue as stated above**

**(*Name and signature of certifying officer*)**

**Name ……………………………  Signature …………………………**

**Station …………………………..  STAMP……………………..Date ……………………**